Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# FIDIA eNEWSLETTER

## Serikali Yaongeza Kiwango cha Pensheni ya Kila Mwezi kwa Wanufaika wa WCF



TOLEO LA SABA | JULAI-OKTOBA 2025 | www.wcf.go.tz

Karibu Sana

# YALIYOMO


- Serikali yaongeza kiwango cha pensheni ya kila mwezi kwa wanufaika wa WCF
- WCF & TUCTA Zaahidi kuendeleza ushirikiano
- Fao la Utengamao Lilivyorudisha Tumaini kwa Wafanyakazi
- WCF yawanoa Madaktari Kuhusu Tahmini za Ulemavu na Magonjwa Yatokanayo na Kazi
- WCF Yang'ara katika Maonyesho ya Biashara Afrika Mashariki
- Habari katika picha


Jarida Mtandaoni
Skanii Kodi ya QR
Hapo Chini


TIMU YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Dkt. John K. Mduma

MHARIRI MKUU
Laura G. Kunenge

MHARIRI MSAIDIZI
Sophia F. Mtakasimba

WACHANGIAJI
Mcharo S. Mrutu
Meseka Z. Kadala
Lilian R. Shembilu

# Dibaji

## Neno Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu

Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha tena katika toleo la pili la jarida letu la mtandaoni kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Jarida hili limekusudiwa kuwa jukwaa la kuwasilisha taarifa muhimu, mafanikio, pamoja na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa manufaa ya wadau wetu wote.

Jarida hili ni nyenzo ya kuimarisha uwazi, uwajibikaji na mawasiliano ya karibu kati ya Mfuko na wadau wetu. Kupitia jarida hili , tunapata nafasi ya kutoa taarifa , kuelimisha juu ya haki na wajibu wa wanufaika, na kuonyesha mchango wa Mfuko katika kuendeleza ustawi wa kijamii na kiuchumi wa Taifa letu.

Katika kipindi hiki, tunayo furaha kuleta habari njema kuhusu ongezeko la kiwango cha pensheni ya kila mwezi kwa wanufaika wa WCF. Hatua hii iliyotangazwa na Serikali ni sehemu ya jitihada endelevu za kuboresha maisha na ustawi wa wanufaika wetu, huku ikidhihirisha dhamira ya Mfuko katika kulinda heshima na maslahi ya wafanyakazi pamoja na familia zao. Ongezeko hili ni ushahidi wa kuimarika kwa mifumo ya hifadhi ya kijamii na jitihada za Serikali kuhakikisha maisha ya wanufaika yanaboreka kadri siku zinavyosonga.

Ninatoa wito kwa wadau wote kuendelea kufuatilia jarida hili na kutumia taarifa zitakazotolewa ili kuongeza uelewa kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi.

Ahsanteni kwa kuendelea kuwa sehemu ya safari ya mafanikio ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

**Dkt. John K. Mduma**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**




# WCF MKONONI APP

## SIFA ZA WCF MKONONI APP

- Mfanyakazi ataweza kujiandikisha, kuingia na kusasisha taarifa za kibinafsi.
- Mfanyakazi ataweza kuona rekodi za mchango wake.
- Mfanyakazi ataweza kupata na kupakua barua mbalimbali kupitia mfumo
- Mfanyakazi ataweza kuwasilisha na kufuatilia madai ya fidia.
- Mfanyakazi ataweza kuwasiliana moja kwa moja na mfuko
- Mfanyakazi ataweza kuwasilisha maswali na mrejesho

# SERIKALI YAONGEZA KIWANGO CHA PENSHENI YA KILA MWEZI KWA WANUFAIKA WA WCF

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetangaza rasmi kuongezeka kwa kiwango cha pensheni ya kila mwezi kwa wanufaika wake. Hatua hii imethibitishwa kupitia notisi ya nyongeza iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, Toleo Na. 319 la tarehe 19 Juni 2025, iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.).

Ongezeko hili linatarajiwa kuwasaidia wanufaika kukabiliana na changamoto za gharama kubwa za maisha zinazoongezeka kila siku. Ni faraja kubwa kwa wanufaika ambao mara nyingi hukabiliwa na mahitaji ya chakula, makazi na huduma za msingi kwa familia zao. Vilevile, ni ishara ya uimara wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katika kutimiza dhamira yake ya kutoa ulinzi wa kijamii (social security protection) kwa Watanzania.

Akizungumza kuhusu maboresho hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo Dkt. John Mduma alisema kuwa ongezeko la pensheni ni hatua muhimu inayolenga kuboresha maisha ya wanufaika pamoja na familia zao, sambamba na kulinda heshima ya mfanyakazi aliyepata madhara kazini, au wategemezi wa mfanyakazi aliyefariki kutokana na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi.

Kwa mujibu wa maelezo yake, nyongeza ya malipo ya pensheni ya kila mwezi imefanyika kwa kuzingatia viwango vya nyongeza vilivyopitishwa kwenye notisi tajwa na mwaka wa ajali, ugonjwa au kifo kinachotokana na kazi kilivyotokea.

Mmoja wa wanufaika wa pensheni ya kila mwezi wa WCF, Bi. Beatrice Masawe, alisema maboresho hayo yameimarisha uaminifu wa wananchi kwa Mfuko huo.

## VIWANGO VYA NYONGEZA YA FIDIA

| No | Mwaka wa Tukio la Ulemavu wa Kudumu au Kifo | Kiwango cha nyongeza (%) |
|---|---|---|
| 1 | 2016-2017 | 31.3 |
| 2 | 2017-2018 | 26.3 |
| 3 | 2018-2019 | 22.3 |
| 4 | 2019-2020 | 19 |
| 5 | 2020-2021 | 15.2 |
| 6 | 2021-2022 | 12 |
| 7 | 2022-2023 | 7.8 |
| 8 | 2023-2024 | 3 |

Kutoka Ukurasa wa 01

Ameeleza kuwa hatua hiyo imejenga picha chanya ya WCF kama taasisi makini inayosimamia rasilimali za wanachama wake kwa uwazi na kwa manufaa ya jamii.

"Ongezeko la pensheni linawawezesha wanufaika kuongeza matumizi, jambo linalochochea mzunguko wa uchumi wa ndani. Hii pia ni fursa kwa sekta ndogo ndogo za biashara kunufaika kutokana na ongezeko la matumizi ya wanufaika," alisema Bi. Beatrice Masawe..

Aidha, alitoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na watendaji husika kwa kusimamia mchakato huo hadi kufanikisha nyongeza ya viwango vya pensheni.

## *Fidia Mtandaoni*
## *https://wwww.portal.wcf.go.tz*



# WCF NA TUCTA ZAAHIDI KUENDELEZA USHIRIKIANO KATIKA UTENDAJI KAZI

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini (TUCTA) wameahidi kuimarisha ushirikiano na umoja katika utendaji kazi na utoaji wa elimu kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na taasisi hizo.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni jijini Dodoma wakati wa semina kwa watendaji wa vyama vya wafanyakazi vilivyo chini ya mwamvuli wa TUCTA kuhusu kazi na huduma zinazotolewa na WCF pamoja na kubadilishana uzoefu juu ya namna ya kuboresha ushirikiano katika utendaji kazi. Semina hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa kutoa elimu kwa wadau kwa mwaka wa fedha 2025/26.

Akizungumza wakati wa kufunga semina hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema kuwa taasisi hizo mbili zimekuwa na historia ya kushirikiana katika masuala yanayozihusu katika utendaji kazi, na kuahidi kuwa Mfuko huo utaendelea kuimarisha ushirikiano huo wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yake.




*Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, akizungumza wakati wa kikao kazi cha Viongozi wa vyama vya wafanyakzi nchini, jijini Dodoma hivi karibuni.*




*Raisi wa TUCTA, Comrade Tumaini Nyamhokye, akisalimia wakati wa kikao kazi cha viongozi wa vyama vya wafanyakazi nchini, jijini Dodoma hivi karibuni.*

TUCTA na wafanyakazi kwa ujumla wamekuwa wadau wakuu wa WCF na mmekuwa mabalozi wetu wazuri katika maeneo na majukwaa mbalimbali. Hivyo, ninawaahidi kuwa WCF tutaendelea kuimarisha ushirikiano na umoja wetu huu katika kutekeleza majukumu yetu kwa weledi," alisema Dkt. Mduma.

Awali, Rais wa TUCTA, Bw. Tumaini Nyamhokye, aliipongeza WCF kwa kuwa na wazo la kufanya semina ya kutoa elimu kwa viongozi wa vyama vya wafanyakazi nchini kwa kuwa hatua hiyo itawawezesha washiriki kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu huduma zinazotolewa na Mfuko huo, na hivyo kuwa mabalozi wazuri kwa wanachama wao.

"Kikao cha namna hii ni muhimu sana kwa kuwa washiriki wote hapa ni viongozi na wawakilishi wa wafanyakazi nchini, hivyo elimu watakayoipata hapa itawawezesha kuisambaza kwa urahisi kwa wanachama wao kupitia njia mbalimbali za mawasiliano," alisema Bw. Nyamhokya.

Semina hiyo iliyohudhuriwa na washiriki takribani 40 kutoka vyama 16 vilivyo chini ya mwamvuli wa TUCTA, ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa WCF wa kutoa elimu kwa wadau kwa mwaka wa fedha 2025/26.





*Afisa Tathmini Madai Mwandamizi, Dkt. Kyangwe Wambura wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, akiwasilisha mada wakati wa kikao kazi cha viongozi wa vyama vya wafanyakazi nchini, jijini Dodoma hivi karibuni.*




Afisa Madai Mwandamizi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Bi. Elice Temu, akiwasilisha mada kuhusu ongezeko la pensheni kwa wafanyakazi

*Rais wa TUCTA, Bw. Tumaini Nyamhokya akiwaongoza washiriki kuimba wimbo wa Mshikamano*





# FAO LA UTENGEMAO LILIVYORUDISHA TUMAINI KWA BECKAM

**Na Mwandishi Wetu**

Kuna usemi wa Kiswahili unasema, "Ajali haina kinga." Katika harakati za maisha ya kila siku, binadamu hukimbizana na majukumu ya kutafuta kipato bila kujua kesho yake itakuwa vipi.

Ni simulizi ya maelfu ya wafanyakazi nchini ambao huamka kila alfajiri, kuingia viwandani, migodini, mashambani au maofisini, wakiwa na ndoto ya kuwaletea familia zao maisha bora.

Lakini dakika chache tu zinaweza kubadilisha maisha ya mtu milele.Hii ndiyo hadithi ya Beckam Martin, kijana aliyekuwa akifanya kazi katika kiwanda cha nondo jijini Dar es Salaam.

Siku moja, akiwa kazini alipata ajali iliyosababisha, mashine kubwa iliteleza ghafla na kumuangukia, na kwa sekunde chache, ndoto azake zote zilitetemeka. Beckam alipoteza mguu wake baada ya kuchomwa na nondo, huo ukawa mwanzo mpya wa maisha ya kijana huyu.

Licha ya maumivu makali aliyopata kutokana na ajali hiyo kichwani mwake alikuwa na mawazo mazito kuhusu hatma ya maisha yake baada ya kupoteza kiungo chake.

"Nitaendesha vipi familia yangu bila uwezo wa kufanya kazi kama zamani?" Itakuwaje maisha bila mguu, kwa kifupi nilikata tamaa ya maisha, niliona mwisho wangu umefika na familia yangu inatumbukia gizani."anasimulia Beckam.

Hata hivyo mawazo hayo hayakudumu kwa muda mrefu maana alitaarifiwa na mwajiri wake kuwa taarifa za ajili yake zimewasilishwa Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi (WCF) ambao ndio watakaosimamia matibabu yake na mafao mengine atakayostahili.

Nilianza Matibabu chini ya uangalizi wa WCF, baada ya kumaliza sasa matibabu yangu madaktari walithibitisha kuwa nina ulemavu wa kudumu hivyo walinijumuisha katika orodha ya wanufaika na nikaanza kunufaika na pensheni ya kila mwezi.

"Nilipata matibabu na hata ilipoonekana nahitaji kuwekewa mguu wa bandia mfuko uligharamia huduma hiyo, haikuishia hapo ninapohisi maumivu nawafahamisha wao wanabeba jukumu la kugharamia huduma za matibabu,"

Beckam anakiri kuwa bila msaada huo familia yake ingekuwa tegemezi, fidia anayopokea inampa uhakika kwamba familia yake haitapoteza mwelekeo.

Kwa kawaida mfanyakazi aliyepata ulemavu wa kudumu anaweza kudhani kuwa hana nafasi tena katika jamii. Lakini kupitia fao la utengamao anaweza kuishi kwa heshima, bila kulazimika kuwa ombaomba mitaani au kutegemea misaada ya majirani na ndugu pekee.

Kwa upande wa Beckam, aliamua kujiajiri akijihusisha na ufundi umeme wa majumbani. Ingawa hawezi tena kurudi kiwandani, sasa anashiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwa namna nyingine. Hii ni ishara kwamba fao la utengamao si msaada wa muda mfupi pekee, bali pia ni chachu ya maisha mapya.

"Maisha ya mtu aliyepoteza kiungo cha mwili hubadilika sana, na mara nyingi huzuni huambatana na msongo wa mawazo hii ndiyo hali niliyopitia awali lakini mawazo haya yalifutika baada ya kuanza kujua kwamba sikutelekezwa na mfumo wa ajira, na kwamba jasho langu la kazi limehifadhiwa kupitia mfuko wa fidia, kulinipa moyo mpya wa kuendelea kuishi.

Kutoka Ukurasa wa 05

"Kwa sababu hiyo niwasihi wafanyakazi kuuchukulia kwa uzito mfuko wa WCF, hakuna anayeijua kesho yake lolote linaweza kutokea sasa pale litakapotokea isiwe mwisho wa maisha au mwanzo wa familia yako kutaabika," anasema Beckam.

Beckam anasisitiza kuwa kila mwajiri na mfanyakazi anapaswa kutambua thamani ya mfuko huu, kuhakikisha michango inalipwa kwa wakati na taratibu zote zinafuatwa.
Kwa kufanya hivyo, endapo ajali itatokea, mfanyakazi hatabaki gizani, bali ataendelea kuishi maisha yenye heshima, matumaini na thamani ya kibinadamu.

## FAO LA UTENGEMAO NI NINI?

Kabla ya kujua fao la utengamao ni muhimu kufahamu maana ya utengaamo. Utengamao ni mkusanyiko wa huduma zinazolenga kuboresha ufanisi wa kazi za kila siku mtu aliyeathirika kibaiolojia (kimaumbile/kiakiri) kwa kumsaidia kupona au kumudu, kufikia kiwango cha juu cha ufanisi cha ushiriki katika kazi mbalimbali za uzalishaji, mafunzo na shughuli mbalimbali za kijamii.

Fao la utengamao ni mojawapo ya mafao saba yanayotolewa na WCF mengine yakiwa huduma ya matibabu, malipo ya ulemavu wa muda mfupi, malipo ya ulemavu wa kudumu, malipo kwa anae mwangalia mgonjwa, malipo kwa wategemezi na msaada wa mazishi.

Aina za utengamao zinazotolewa katika fao hili ni utengamao wa kitabibu (clinical rehabilitation), Utengamao wa ujuzi na kazi (vocational rehabilitation), na Utengamao wa kijamii (social rehabilitation).

Kwa mujibu wa ofisa tathmini wa WCF, Dk Kyangwe Wambura tangu kuanza kutoa mafao, mfuko umekuwa ukitoa utengamao wa kitabibu lakini sasa sheria imesainiwa kuruhusu kutolewa utengamao wa kijamii na utengamao wa ujuzi na kazi.





Madhumuni mengine ni kumjengea mhanga uwezo wa kushiriki katika kazi za kujipatia kipato na kumwezesha mhanga kushiriki katika shughuli za kijamii.



# WCF YAWANOA MADAKTARI KUHUSU TATHMINI ZA ULEMAVU WA MAGONJWA YATOKANAYO NA KAZI.





*Baadhi ya Madaktari wakifanya mafunzo kwa vitendo*

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeendesha mafunzo kwa madaktari kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Mwanza, yalilenga katika kuwaongezea wataalamu hao weledi katika kufanya tathmini ya ulemavu wa magonjwa yatokanayo na kazi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wafanyakazi wanaopatwa na changamoto hizo.

Akifungua rasmi mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Mhe. Amir Mkalipa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda, alisisitiza umuhimu wa madaktari kupata uelewa wa kitaalamu kuhusu masuala ya afya ya wafanyakazi, akieleza kuwa ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha haki za wafanyakazi zinazingatiwa kupitia tathmini sahihi za kitabibu.

"Serikali inatambua mchango mkubwa wa WCF katika kulinda ustawi wa wafanyakazi, mafunzo haya yatawawezesha madaktari kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu namna ya kufanya tathmini ya ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi jambo litakalosaidia kuongeza idadi ya madaktari wenye ujuzi wa kufanya tathmini na kufikia maamuzi ya kitabibu, yanayohusika na fidia za ulemavu hivyo kulinda nguvu kazi ya taifa" alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa WCF Bw. Anselim Peter, alibainisha kuwa taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na wataalamu wa afya katika kuhakikisha wafanyakazi wanapata huduma bora na kwa wakati.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini WCF, Dkt. Abdulsalaam Omary amesema kuwa dhamira ya WCF ni kuongeza idadi ya madaktari wanaopata mafunzo ya aina hiyo katika maeneo mbalimbali nchini ili kuendeleza ulipaji wa Fidia stahiki.



*Afisa Tathmini Madai Mwandamizi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Dkt. Sweetberth Sambala akitoa maelekezo wakati wa mafunzo kwa vitendo*

Mmoja wa washiriki wa Mafunzo hayo Dkt. Pius Kagoma alipongeza jitihada za WCFkuwafikia wataalamu hao huku akieleza kuwa mafunzo hayo yanawajengea uwezo wa kufanya tathmini Madaktari kwa kuzingatia viwango ambapo wakirudi katika maeneo yao ya kazi wataweza kuwatambua wafanyakazi wanaopata magonjwa au ajali zitokanazo na kazi na wataweza kufidiwa na WCF hivyo kuweza kurudi katika kazi za ujenzi wa Taifa.




*Baadhi ya Madaktari kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kukamilika kwa mafunzo kwa vitendo na namna ya kuyabaini magonjwa yatokanayo na kazi. Mafunzo yaliyotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)*




*Baadhi ya Madaktari kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa wakiwa kwenye picha ya pamoja na mgeni rasmi Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Amir Mkalipa na Baadhi ya Viongozi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi*

# WCF YANG'ARA KATIKA MAONESHO YA 20 YA BIASHARA YA AFRIKA MASHARIKI JIJINI MWANZA.




*Afisa Mfawidhi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Kanda ya Ziwa Bwana Joseph Siri, akipokea tuzo kutoka kwa Rais wa Chemba ya Viwanda, Biashara na Kilimo Tanzania (TCCIA), baada ya WCF kuibuka mshindi wa Nafasi ya Pili katika kipengele cha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwenye Maonesho ya 20 ya Biashara ya Afrika Mashariki.*

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeshiriki Maonyesho ya 20 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyamagana, jijini Mwanza, Agosti 29 hadi 07 Septemba, 2025.

Maonesho hayo yalifunguliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda, ambapo WCF ilitunukiwa tuzo ya mshindi wa pili katika kundi la waonyeshaji wa sekta ya Hifadhi ya Jamii. Tuzo hiyo ni ishara ya kutambua mchango na ubora wa huduma ambazo Mfuko uliendelea kuwapatia wananchi waliotembelea banda lake.

Kupitia ushiriki wake katika maonyesho hayo, WCF ilitumia fursa hiyo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu shughuli za mfuko ikiwemo, mafao yanayotolewa, taratibu za kuwasilisha madai na pia namna ya kutumia mifumo ya kidijitali ikiwemo Fidia App na WCF portal kufuatilia madai au kutambua kama mwajiri anawasilisha michango ya kila mwezi katika Mfuko.

Idadi kubwa ya wananchi walitembelea banda la WCF kutokana na ubora wa huduma zilizokuwa zinatolewa na wataalamu wa WCF.






# HAPPY CORNER



# HABARI KATIKA PICHA






















Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA